# HALMASHAURI YA WILAYA YA HAI

## KIJIJI CHA NRONGA

S.L.P. 3023 MOSHI

**STAKABADHI YA MICHANGO YA KIJIJI**

No. 0841

Tarehe: 13.3.2023

Nimepokea kutoka kwa ALTEZA TRAVELLING

Kiasi cha Shilingi MILIONI MOJA NA LAKI MBILI

Kwa ajili ya malipo ya USHURU WA KIJIJI (SHAMBA

Ahsante

Taslimu / Hundi No. —

Shs. 1,200,000/=

[signature]

Sahihi ya Mpokeaji

SHERIA YA ARDHI NO. 4 YA 1999

---------------------------

# MKATABA WA MAUZO YA SHAMBA

## KATI YA

## AKALUUFOO MEZAKI LEMA, (MUUZAJI)

## NA

## ALTEZZA TRAVELLING LIMITED(MNUNUZI)

**Umetayarishwa na:**

**PANDE ZOTE HUSIKA**

**11 Februari, 2023**

# MKATABA WA MAUZO YA SHAMBA

Mkataba huu umesainiwa leo tarehe 11 Februari, 2023.

**KATI YA**

**AKALUUFOO MEZAKI LEMA** wa kijiji cha Nronga mwenye kitambulisho chenye namba ya usajili 19520323-25312-00001-25, Tanzania, (hapa anajulikana kama "**Muuzaji"** ambaye hapa itawajumuisha kama itakavyoonekana na itakavyojulikana itawahusisha vile vile warithi na wahusika wote wa ***Muuzaji*** kwa upande mmoja).

**NA**

**ALTEZZA TRAVELLING LIMITED** kampuni yenye namba za usajili wa Brela namba 107456 na TIN 124-524-008 ya Sanduku la Posta 938 Kilimanjaro, Tanzania, (hapa kujulikana kama "**Mnunuzi"** ambaye hapa itawajumuisha kama itakavyoonekana na itakavyojulikana itawahusisha vile vile wahusika wote wa ***Mnunuzi*** kwa upande wa pili).

**UTANGULIZI**

**KWAMBA** Muuzaji ni mmiliki halali wa shamba lenye ukubwa wa mita 37 upande wa magharibi yani kutokea mtoni,upande wa kusini mita 170, upande wa mashariki 32,upande wa Kaskazini 170, kijiji cha Nronga, wilaya ya Hai, Mkoa wa Kilimanjaro.

**Viwianishi vya GPS vya shamba:**

3°10'0.25"S 37°13'1.28"E
3° 9'59.90"S 37°13'4.40"E
3° 9'59.78"S 37°13'6.66"E
3°10'0.87"S 37°13'6.59"E
3°10'0.75"S 37°13'4.27"E
3°10'1.38"S 37°13'1.31"E

*Saini ya Muuzaji*..........................

*Saini ya Mnunuzi*..........................

Upande wa Mashariki limepakana na eneo la Exzaudi Meshack Lema;
Upande wa Magharibi limepakana na mto;
Upande wa Kaskazini limepakana na eneo la Sariandumi Emmanuel Kweka;
Upande wa Kusini limepakana na eneo la Exzaudi Obadia Lema.

**KWAMBA,** Muuzaji kwa kujua, kwa kukusudia, akiwa na akili yake timamu na kwa hiari yake mwenyewe anadhumuni la kuuza shamba kwa mnunuzi ikiwa ni kwa kuzingatia masharti yaliyo ainishwa kwenye mkataba huu. Muuzaji ni mmiliki halali wa shamba lenye ukubwa wa mita 37 upande wa magharibi yani kutokea mtoni,upande wa kusini mita 170, upande wa mashariki 32,upande wa Kaskazini 170, kijiji cha Nronga, wilaya ya Hai, Mkoa wa Kilimanjaro.

**NA KWAMBA** Mnunuzi hapa anakusudia kununua shamba hilo kwa malipo ya **Shilingi za Kitanzania milioni kumi na mbili (12,000,000/=) tu.**

**MKATABA HUU WA MAUZIANO UNASHUHUDIA KWAMBA:-**

**1.0 BEI YA MANUNUZI**

1.1 Kwa makubaliano ya Muuzaji kupewa **Shilingi za Kitanzania Milioni kumi na mbili (12,000,000.00) tu** ikiwa ni bei iliyokubaliwa kwa ajili ya mauziano ya ardhi iliyotajwa hapo juu, Muuzaji hapa anakubali na kumuuzia mnunuzi eneo la ardhi lililotajwa hapa juu ikiwa ni pamoja na maendelezo yote yaliyopo kwenye eneo hilo la ardhi.

1.2 Muuzaji na Mnunuzi wamekubaliana kuwa bei hii ya ununuzi wa eneo hilo lililotajwa hapo juu yani **Shilingi za Kitanzania Milioni kumi na mbili (12,000,000.00) tu** zitalipwa kwa Muuzaji na Mnunuzi siku ya kutia sahihi Mkataba huu.

1.3 Pesa italipwa moja kwa moja kwenye akaunti ya mtoto wa muuzaji iliyopo benki ya NBC yenye akaunti namba 057201028067 Yenye Majina ya mtoto wa Muuzaji wa Kiume aitwae Peniel Lema.

*Saini ya Muuzaji*..........

*Saini ya Mnunuzi*..........

1.4 Muuzaji na Mnunuzi wamekubaliana kuwa Muuzaji hatahamisha wala kuondoa kitu chochote, wala mastawisho ya aina yoyote yatakayokuwepo kwenye eneo hilo la ardhi wakati wa makabidhiano ya eneo hilo.

## 2.0 MAELEZO YA ARDHI

Muuzaji ni mmiliki halali wa shamba lenye ukubwa wa mita 37 upande wa magharibi yani kutokea mtoni,upande wa kusini mita 170, upande wa mashariki 32,upande wa Kaskazini 170, kijiji cha Nronga, wilaya ya Hai, Mkoa wa Kilimanjaro.

**Viwianishi vya GPS vya shamba:**

3°10'0.25"S 37°13'1.28"E
3° 9'59.90"S 37°13'4.40"E
3° 9'59.78"S 37°13'6.66"E
3°10'0.87"S 37°13'6.59"E
3°10'0.75"S 37°13'4.27"E
3°10'1.38"S 37°13'1.31"E

## 3.0 MASHARTI YA UNUNUZI

3.1 Kwamba, muuzaji ni mmiliki halali wa shamba lenye ukubwa wa mita 37 upande wa magharibi yani kutokea mtoni,upande wa kusini mita 170, upande wa mashariki 32,upande wa Kaskazini 170, kijiji cha Nronga, wilaya ya Hai, Mkoa wa Kilimanjaro.

3.2 Kwamba hakuna pingamizi lolote wala rehani au zuio lolote la kisheria na endapo itabainika vinginevyo na kutokea mgogoro wowote kuhusiana na eneo hilo, Muuzaji atakabiliana na mgogoro huo kwa gharama zake mwenyewe hadi kufikia mwisho.

3.3 Mkataba huu unashuhudia kuanza kwa umiliki halali wa Mnunuzi wa Shamba hilo na ule wa Muuzaji unakoma mara moja baada ya kusainiwa kwa mkataba huu na kulipwa kwa bei ya ununuzi na Makubaliano haya yatawahusu pia warithi na vizazi vya Muuzaji na Mnunuzi.

*Saini ya Muuzaji.....................*

*Saini ya Mnunuzi.....................*

3.4 Muuzaji hapa anakubali kuwa atakuwa tayari kumlipa Mnunuzi fidia yoyote dhidi ya mashtaka, upotevu, au jukumu lolote linalohusiana na Mkataba huu au litakalokuwa linahusu kipengele chochote cha Mkataba huu.

Fidia hiyo italipwa kutokana na hasara na muda utakaokuwa umepotezwa na Mnunuzi aliyetajwa hapa na kama mashitaka au hasara hiyo inatokana na kuvunjika kwa kipengele chochote cha Mkataba huu.

3.5 Endapo itathibitika kwamba muuzaji sio mmiliki halali wa shamba hili mkataba huu utakuwa batili na muuzaji atawajibika kulipa gharama zote kadri ya mnunuzi atakavyo dhibitisha ikiwa ni pamoja na kurudisha mara mbili ya fedha alizozitoa mnunuzi chini ya mkataba huu kulingana na thamani ya fedha kwa wakati huo.

**4.0 MUUZAJI ANAIDHINISHA KWAMBA**

4.1 Muuzaji anamhakikishia Mnunuzi kama ifuatavyo:

4.1.1 Taarifa zozote zilizotolewa na Muuzaji au kwa niaba yake kwa Mnunuzi katika maelewano ya kufikia kwenye mkataba huu, zilitolewa na zitabakia kuwa kweli na sahihi kwa njia zozote zile na Muuzaji hana jambo lolote lililofichika ambalo litazifanya taarifa hizi kuwa za uongo, hazijakamilika au si sahihi au za kupotosha.

4.1.2 Katika kukamilisha mkataba huu au kutekelezwa kwa vipengele vya mkataba huu hakuna jambo lolote litakaloathiri mkataba wowote ule ambao Muuzaji ni sehemu ya mkataba huo au amri yoyote ya mahakama.

4.1.3 Muuzaji hana ufahamu wowote wa kuingia kwa eneo linalouzwa kwenye ardhi ya mtu mwengine yeyote au jirani nae na kama litakuwepo jambo lolote Muuzaji atahakikisha kuwa anamlipa Mnunuzi fidia ya kitu chochote kitakachojitokeza;

**5.0 WAHUSIKA HAPA WANAKUBALIANA KUWA**

5.1 Mkataba huu unajumuisha vipengele vyote vya Mkataba halisi wa mauziano ya ardhi baina ya wahusika hapa na kuhusiana na jambo linalohusika kwenye Mkataba

*Saini ya Muuzaji*..........

*Saini ya Mnunuzi*..........

huu na hakuna uwasilishi au udhamini wa aina yoyote utakaobana upande wowote kutokana na Mkataba huu au kutokana na kipengele chochote cha Mkataba huu.

5.2 Hakuna Mkataba wowote unaoongeza, unaobatilisha, unaofuta au unaoondoa kipengele chochote cha Mkataba huu isipokuwa mpaka Mkataba huo uwe umewekwa kwenye maandishi na kusainiwa na wahusika hapa au na wawakilishi wao waliokubaliwa kusaini kwa niaba yao.

5.3 Wahusika hapa wamekubali kusaini na kufanya jambo lolote kuhakikisha kuwa Mkataba huu unafanikiwa na kuwekwa saini kama inavyopaswa. Inakubaliwa kwamba kwa wahusika kusaini mkataba huu ni uthibitisho kwamba Muuzaji amepokea fedha kama ilivyoainishwa hapo juu zilizokubaliwa kama malipo ya eneo lililouzwa pamoja na maendelezo yoyote yaliyofanyika kwenye eneo hilo.

**6.0 USULUHISHI**

6.1 Mgogoro wowote utakaojitokeza kutokana au utakaounganishwa kwenye mkataba huu utasuluhishwa pamoja kati ya pande mbili husika, itakaposhindikana, wahusika kwenye mkataba huu watapeleka mashauri yao kwa Msuluhishi kama ilivyoainishwa kwenye Sheria ya Usuluhishi au njia nyingine yoyote ya usuluhishi kama itakavyokubaliwa na pande husika kwenye mkataba huu.

**7.0 MENGINEYO**

7.1 Isipokuwa kama ilivyofafanuliwa kwingineko, ikiwa upande mmoja hautafanya yale yanayopaswa au kutofanya mojawapo ya vipengele vya mkataba huu na ambacho ni haki kukitekeleza hakitaonyesha kuwa upande huo umesamehe au umeepuka kutekeleza haki alizopewa.

7.2 Jambo lolote lililotokea katika mkataba huu au linalohusu mkataba huu litakuwa linaongozwa na kutafsiriwa kwa Sheria za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

7.3 Mkataba huu utakuwa kwa lugha ya Kiswahili na utakuwa katika nakala halisi Tatu.

*Saini ya Muuzaji*...................

*Saini ya Mnunuzi*...................

**KWA USHUHUDA BASI**, pande zote mbili zinazohusika katika Mkataba huu zimeweka saini zao hapa chini kama ifuatavyo:-

Mkataba huu umewekwa saini na kupokelewa na **AKALUUFOO MEZAKI LEMA** leo tarehe 11 Februari 2023. } ....AMLema.... **MUUZAJI**

**Shahidi wa Muuzaji**.

1DRUSNA LEMA (mke wa muuzaji) ..........................

2. PENIEL LEMA (mtoto wa muuzaji) ..........................

ASANTAEL MEZAKI LEMA

**Mbele ya:**

**Jina**.......GEOFREY JOHN.......

**Wadhifa:**.......WAKILI.......

**Tarehe:**.......~~28~~ 11 Februari, 2023.......

**Kamishina wa Kiapo**

Mkataba huu umewekewa saini na kupokelewa na Aleksandr Andreichuk kwa Niaba ya **ALTEZZA TRAVELLING LIMITED** ambaye namjua, leo tarehe 11 Februari 2023. } .......................... **MNUNUZI**

**MBELE YA:**

**JINA**.......GEOFREY JOHN.......

**SAHIHI**..........................

**WADHIFA**.......WAKILI.......

**TAREHE**.......11 Februari, 2023.......

**JINA:** .......Dickson Muganda.......

**SAHIHI**:..........................

**WADHIFA** .......Meneja Miradi.......

**TAREHE**:.......11/02/2023.......

*Saini ya Muuzaji*..........................

*Saini ya Mnunuzi*..........................

**MAKUBALIANO HAYA YAMEHIDHINISHWA NA OFISI YA KIJIJI**

**CHEO** MWENYEKITI

**JINA** VALERIAN A. LEMA

**SAHIHI** ...........................

MWENYEKITI WA
S.L.P. 3023 MOSHI
TAREHE
KIJIJI CHA NRONGA

**CHEO** M/KITONGOJI

**JINA** JULIUS S. LEMA

**SAHIHI** ...........................

*Saini ya Muuzaji*...........................

*Saini ya Mnunuzi*...........................